# Miundo ya Viegesho vya Kiwango katika Sentensi za Kiswahili: Mtazamo wa Nadharia ya Eksibaa

*Mussa Omari Amanzi*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

**Ikisiri**

**Makala yanahakiki viegesho vya kiwango katika sentensi za Kiswahili. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu za hojaji, usaili, ushuhudiaji na usomaji matini ambazo zilihusu ubainishaji wa viegesho vya kiwango. Nadharia ya Eksibaa iliyoasisiwa na Chomsky (1970) imetumiwa kubainisha na kuchambua miundo ya viegesho hivyo. Data zimechanganuliwa kwa kutumia mbinu ya vielelezo vya mchoroti pamoja na maelezo. Matokeo yanadhihirisha kuwa kisintaksia, kuna miundo kumi na nne (14) ya viegesho vya kiwango katika sentensi za Kiswahili. Miundo hiyo imetokana na ushikamani wa viambajengo vinavyounda viegesho vya kiwango katika Kiswahili.**

**Maneno Muhimu:** Miundo, Viegesho, Sentensi, Eksibaa

## Utangulizi na Mapitio ya Maandishi

### Maana na Aina za Viegesho

Kwa kawaida, Kiswahili ni lugha yenye mpangilio wa kitenzi kati, yaani huanza na nomino, kitenzi kisha yambwa tendwa au yambwa tendewa. Pamoja na mpangilio huo, huwa pia kuna taarifa za ziada zinazohusu kitenzi, kiima, yambwa, yambiwa au sentensi nzima. Taarifa hizo za ziada huongezwa kwa kutumia viambajengo mbalimbali ambavyo katika utafiti huu ndivyo vilivyoitwa viegesho. Kwa hiyo, viegesho ni viambajengo vinavyotoa taarifa za ziada baada ya kukamilika mahusiano ya lazima katika vipashio mbalimbali ya lugha. Kwa mfano, katika sentensi *Juma anacheza mpira kwa makini* au *Juma mwenyewe amecheza mpira*, kirai kihusishi **kwa makini**, au kivumishi **mwenyewe** ni viambajengo ambavyo huweza kuondolewa bila ya kuharibu utangamano wa msingi wa vijenzi muhimu wa sentensi husika.

Katika kazi yake inayohusu viegesho katika Kiswahili, Harries (1969) anasema kuwa kiegesho ni kiambajengo kisichokuwa na uhusiano wa moja kwa moja na maneno mengine kisintaksia, bali hufanya kazi ya kutoa taarifa za ziada katika neno au kundi la maneno. Naye Ernst (2004) anasema kiegesho ni kiambajengo kisichokuwa king'oesho katika tungo. Kiegesho huwa na kazi ya kukumusha kirai nomino au kirai kitenzi.

Kuna aina mbalimbali za viegesho, kama vile viegesho vya namna, wakati, mahali, ala, sababu na kiwango. Kwa kuwa kazi hii inahusu viegesho vya kiwango; hivyo tutaeleza maana ya viegesho vya kiwango pekee. Zipo kazi chache za kitafiti

zinazoeleza viegesho vya kiwango lakini si kwa upekee wake bali kwa kuviweka katika kapu moja la viegesho kwa ujumla. Mgonja (1985:26) anaeleza kuwa viegesho vya kiwango ni vile ambavyo huonesha "ni kwa kiwango gani tukio limefanyika". Kwa mfano, *watu wengi walipenda sana wimbo huu*. Neno *sana* katika mfano huu ni kiegesho cha kiwango. Huddleston na Pullum (2006) wanaeleza kuwa viegesho vya kiwango ni vile vinavyoeleza kiwango cha ubora, idadi, ukubwa na uzito.

Zipo tafiti mbalimbali duniani zilizochunguza viegesho katika lugha tofautitofauti. Arts (1977), Dembetembe (1987) na Tallerman (2005) ni baadhi ya wanaisimu waliofanya tafiti linganishi kuhusu viegesho na vijalizo. Katika tafiti zao, wote wanakubaliana kuwa kiegesho ni kiambajengo cha hiari katika tungo wakati wote lakini kijalizo ni kiambajengo cha lazima katika tungo. Kijalizo hujaliza neno kuu na huwa karibu na neno hilo wakati kiegesho hakina uhusiano wa karibu na neno kuu. Kiegesho kinaweza kuhamahama katika sentensi/kishazi kwa kuwekwa mwanzoni, kati au mwishoni lakini kijalizo huwa hakina sifa ya kuhamahama.

**Uchunguzi wa Viegesho katika Kiswahili**

Katika Kiswahili, viegesho havikuchunguzwa kwa kiasi kikubwa. Kwa sababu hiyo, hakuna kazi nyingi za kitafiti zinazoeleza viegesho. Miongoni mwa tafiti chache zilizofanyika ni pamoja na zile za Harries (1969) na Mgonja (1985). Hawa wanavieleza viegesho kwa kuvijumuisha na vijalizo na vielezi. Katika kazi hizo, wataalamu hawa wanaeleza moja kwa moja kuwa kiegesho ni kielezi. Mifano iliyotumika katika kueleza viegesho hivyo ni mifano ya vielezi pekee. Pia, katika kazi hizo, viegesho havitofautishwi na vijalizo. Kwa mfano, katika maelezo yake, Mgonja (1985) anakubali kuwa kiegesho ni kiambajengo cha hiari lakini wakati mwingine kiambajengo hichohicho hujitokeza kama kijalizo. Mgonja akitumia mfano huu, *Muhujumu amepelekwa mahakamani*, anaeleza kuwa kiambajengo *mahakamani* ni kielezi cha lazima kwa kuwa kinajibu swali la wapi. Huku ikichukuliwa kuwa viambajengo vinavyojibu swali la wapi, namna gani, mara ngapi na wakati gani ni vielezi, ilhali maswali hayo yanaweza kujibiwa na viambajengo vingine. Hivyo, kwa kuwa amekiita kiambajengo hicho ni kielezi cha lazima basi akahitimisha kuwa ni kiegesho cha lazima. Kwa hakika, kiambajengo hicho si kielezi kwa sababu hakipo katika mahusiano ya hiari, bali ni nomino ya mahali kwa kuwa ni kijalizo cha kitenzi *peleka*. Kwa hiyo, kiambajengo cha lazima kinachotoa maana ya msingi, na si ya ziada, huitwa kijalizo na si kiegesho.

Vielezi na viegesho si dhana sawa. Kila moja inatofautiana na nyingine. Kwa hiyo, utafiti huu umekubaliana na maelezo ya Harries (1969) na Mgonja (1985) kuwa baadhi ya vielezi ni viegesho ila unatofautiana na maelezo yao kuwa viegesho ni vielezi. Katika sarufi mapokeo, kategoria ya vielezi ndiyo iliyoonekana kufanya kazi ya kutoa taarifa za ziada katika sentensi. Hivyo, kategoria ya vielezi pekee ndiyo iliyochunguzwa kama viegesho. Nadharia ya Eksibaa ndiyo iliyokuja

kuieleza kiundani dhana ya viegesho, tofauti na mtazamo wa awali. Ikabainika kuwa viegesho siyo vielezi tu, vinaweza kuwa vihusishi, vivumishi, vibainishi na kadhalika. Freidin (1992) anakichukulia kirai kibainishi kuwa ni kiegesho, na kukiita kirai kiegesho. Vallin (2001) anasema kirai kihusishi kinaweza kuwa kiegesho au kijalizo. Kinakuwa kijalizo ikiwa ni mahusiano ya lazima na kinakuwa kiegesho ikiwa ni mahusiano ya hiari kisemantiki au kisintaksia.

Viegesho vya kiwango kama vilivyo vipashio vingine katika lugha huwa na dhima ya kufafanua taarifa, kupamba lugha, kuonesha msisitizo, namna, kuelezea idadi na kadhalika. Kwa ujumla, viegesho ni viambajengo muhimu sana kimuundo ili kupata maana ya ziada baada ya mpangilio wa mahusiano ya lazima katika sentensi. Kwa hiyo, lengo la makala hii ni kubainisha viegesho vya kiwango pamoja na miundo yake katika sentensi za Kiswahili.

**Nadharia ya Eksibaa**

Nadharia ya Eksibaa iliasisiwa na Chomsky (1970) ambaye ndiye mwasisi wa Nadharia ya Sarufi Miundo Virai. Nadharia ya Sarufi Miundo Virai imetoa mchango mkubwa sana katika sintaksia kwa kuchunguza kategoria za virai katika sawia mbili ambazo ni kategoria za kiwango cha neno na kiwango cha kirai. Katika miaka ya 1970, Chomsky aligundua kuwa Nadharia ya Sarufi Miundo Virai ina upungufu katika kuainisha kategoria za virai kwa kuwa ina sawia mbili tu ambazo ni XP na P ilhali katika tungo kuna kirai kikubwa kuliko neno (P) na kidogo kuliko kirai (XP). Pia, Nadharia ya Sarufi Miundo Virai, kwa kuwa ina sawia mbili tu inashindwa kutofautisha mahusiano ya lazima katika virai na mahusiano ya hiari, kwa kuwa sawia mbili hazitoshi kuonesha uhusiano huo. Vilevile, Nadharia ya Sarufi Miundo Virai ina kanuni nyingi zinazohusisha kategoria tofautitofauti, hivyo ikaonekana ni lazima kuwa na kanuni chache.


Kutokana na upungufu huo, Chomsky (1970) akaiboresha nadharia hiyo kwa kuongeza sawia ya kati, na kuibuka na Nadharia ya Eksibaa. Inaitwa Nadharia ya Eksibaa kwa sababu inatumia msimbo X ambao unawekewa baa (¯au′) juu ya X. Nadharia hii inatatua matatizo yaliyojitokeza katika Nadharia ya Sarufi Miundo Virai, kama inavyooneshwa hapo juu.

Nadharia ya Eksibaa imeongeza sawia ya kati ambayo ni kategoria kubwa kuliko neno na ni ndogo kuliko kirai. Radford (1988) ametumia mfano wa *the king of Jen* kuonesha kuwa *king of Jen* katika Nadharia ya Eksibaa, ni kirai kikubwa kuliko nomino lakini ni kidogo kuliko kirai kikuu chote. Kwa hiyo, kwa kuongozwa na Nadharia ya Eksibaa, virai vinaainishwa katika sawia tatu, ambazo ni XP, P′, P. Hivyo, baada ya kuwa na kanuni nyingi, Nadharia ya Eksibaa inatupatia kanuni chache zinazoeleza miundo mingi.

Haegeman (1994) katika kuieleza Nadharia ya Eksibaa, anasema kuwa, virai vyote ni lazima vibebwe na kirai kikuu kimoja. Hivyo, katika mahusiano ya virai, kijalizo huwa kinaungana na X kuunda X′ na kiegesho huwa kinaungana na X′ kuunda X′. Aidha, kibainishi huwa kinaungana na X′ kuunda XP. Kwa ujumla,


Nadharia ya Eksibaa imesaidia sana kuonesha uhusiano wa viambajengo mbalimbali vya virai. Vipo vile vyenye uhusiano wa lazima na vipo vile vyenye uhusiano wa hiari. Vielelezo vifuatavyo, vitatusaidia kuweka wazi zaidi mahusiano hayo:

**Kielelezo Na 01: Vijalizo katika Mahusiano ya Virai**




Katika kielelezo hichi, tunaweza kupata kanuni ifuatayo: X′ —> X ... KIJALIZO, yaani kiambajengo mama cha X′ kikizaa kiambajengo binti cha X ziro, hivyo kiambajengo dada cha kiambajengo binti hicho ni kijalizo, ambapo haya ni mahusiano ya lazima.

**Kielelezo Na 02: Viegesho na vijalizo katika mahusiano ya virai**




Katika kielelezo hapo juu, tunaweza kuwa na kanuni ifuatayo: X′ —> X′ ... KIEGESHO, yaani kiambajengo mama cha X′ kikizaa kiambajengo binti cha X′. Hivyo kiambajengo dada cha kiambajengo binti hicho ni kiegesho, ambapo haya ni mahusiano ya hiari.


Msingi mwingine wa Nadharia ya Eksibaa ni kuainisha miundo ya virai kwa kuzingatia neno kuu la kirai na vijalizo vyake. Nadharia hii hutumika kuelezea miundo ya virai kama ilivyo Nadharia ya Sarufi Miundo Virai, kwa kuwa nadharia hii ni maboresho tu ya Nadharia ya Sarufi Miundo Virai (Black, 1999). Nadharia ya Eksibaa inayoweka wazi miundo mbalimbali ya virai inaonesha namna virai hivyo

vinavyoundwa kupitia msingi wake wa kuainisha virai kwa kuzingatia neno kuu la kirai na vijalizo vyake. Kwa kuwa viegesho vinaundwa na virai, virai hivyo vimechunguzwa neno lake kuu na vijalizo vyake ili kupata muundo wake.

**Ubainishaji wa Viegesho katika Kiswahili**

Katika kubainisha viegesho kwa ujumla, mbinu kubwa iliyotumika katika utafiti huu ni kutumia kanuni ya Nadharia ya Eksibaa inayotofautisha mahusiano ya lazima na mahusiano ya hiari. Kwa mujibu wa Nadharia ya Eksibaa, viegesho hujitokeza katika kanuni ya mahusiano ya hiari. Kanuni inayotumika katika Nadharia ya Eksibaa kubainisha viegesho ni X′ —> X′ **(ZP)**... KIEGESHO.

**Kielelezo Na. 03: Viegesho katika Mahusiano ya Virai**




Katika kanuni hii ya mahusiano ya hiari, kiambajengo binti cha X′ kinashirikiana na kiambajengo dada cha ZP kuunda kiambajengo mama cha X′. Hivyo, katika uhusiano wa namna hii, kiambajengo binti kinachounda kiambajengo mama huwa kimeshajitosheleza kimuundo kuunda kiambajengo mama hicho. Hivyo, kiambajengo dada huwa ni muundo wa ziada tu katika kiambajengo binti katika kuunda kiambajengo mama. Kwa hiyo, kiambajengo dada katika mahusiano ya namna hii, huitwa kiegesho. Turejelee mfano ufuatao:

| |
|---|
| Nitampiga adui yangu kwa kadiri niwezavyo |

Chanzo cha Data: Mtafiti (2020)


Katika data hii, kirai kitenzi kikuu (*nitampiga adui yangu kwa kadiri niwezavyo*) kimeundwa na viambajengo vitatu ambavyo ni (*nitampiga*), (*adui yangu*) na (*kwa kadiri niwezavyo*). Viambajengo hivyo vimegawanyika katika sehemu mbili, (*nitampiga adui yangu*) na (*kwa kadiri niwezavyo*). Hii ni kwa sababu kirai nomino (*adui yangu*) kinabebwa ndani ya kirai kitenzi cha kati T′ (*nitampiga adui yangu*). Kirai kihusishi (*kwa kadiri niwezavyo*) ni kirai kinachoshirikiana tu na kirai kitenzi hicho cha kati kuunda kirai kitenzi kikubwa zaidi T′ kilichotokana na kirai kitenzi kikuu KT.

Kwa hiyo, mahusiano ya kirai kihusishi na kirai kitenzi cha kati katika data hiyo ni ya hiari kwa kuwa kirai kitenzi cha kati (*nitampiga adui yangu*) kimeshajitosheleza kimuundo. Hivyo, kirai kihusishi (*kwa kadiri niwezavyo*) kinaongeza taarifa za ziada tu katika muundo huo. Hivyo, kirai kihusishi hicho ni

kiegesho. Mfano huo unaweza kufafanuliwa zaidi kwa kutumia kielelezo cha matawi, kama ifuatavyo:

**Kielelezo Na. 04: Mfano wa Kiegesho**

**Nitampiga adui yangu kwa kadiri niwezavyo**




Katika Kielelezo hapo juu, kirai (KH) ni kiambajengo dada cha kirai (T′) cha upande wa kushoto lakini pia ni kiambajengo binti cha kirai (T′) kilichopo juu. Hivyo, kirai (KH) kinashirikiana na kirai (T′) cha upande wa kushoto kuunda kirai (T′) cha juu kinachotokana na kirai (KT). Uhusiano huu wa kirai (KH) na kirai (T′) kuunda kirai (T′) ni wa hiari kimuundo. Hivyo kirai (KH) ni kiegesho.


Baada ya ufafanuzi huo unaohusu viegesho kwa ujumla, ni vizuri tukaichunguza tena data ifuatayo:

| |
|---|
| Nitampiga adui yangu kwa kadiri niwezavyo |

Chanzo cha Data: Mtafiti (2020)

Katika data hii, sentensi imeundwa na kirai kitenzi (*nitampiga adui yangu*), kirai kihusishi (*kwa kadiri niwezavyo*) na kirai nomino (*adui yangu*). Kirai kihusishi ni kiegesho kwa kuwa kipo katika mahusiano ya hiari kimuundo katika tungo hiyo kama ilivyofafanuliwa hapo juu. Lakini katika data hiyo, kirai nomino (*adui yangu*) ni kijalizo kwa kuwa kipo katika mahusiano ya lazima kimuundo katika tungo hiyo. Kirai nomino (adui yangu) hakiwezi kuondolewa kutoka katika kisabiki chake ambacho ni kitenzi (nitampiga) na sentensi hiyo ikababakia imara kimuundo. Uhusiano huu wa lazima unaweza kufafanuliwa zaidi katika kielelezo kifuatacho:

**Kielelezo Na 05: Mfano wa Kijalizo**
**Nitampiga adui yangu kwa kadiri niwezavyo**




Kiambajengo (KN) katika kielelezo hapo juu, ni kijalizo na siyo kiegesho, kwa sababu virai T + KN vinabebwa na kuzaliwa na kiambajengo mama ambacho ni kirai cha kati T′**.** Kwa hiyo, T + KN vinashirikiana na kutegemeana katika kuunda maana ya msingi katika kirai hicho cha kati. Hivyo, huwa ni mahusiano ya lazima.

Hivyo, dhana ya viegesho inatofautiana na dhana ya vijalizo kwa kuzingatia uhusiano wa viambajengo katika tungo. Viambajengo vinapojitokeza katika uhusiano wa hiari ni viegesho na katika uhusiano wa lazima ni vijalizo.

Baada ya ufafanuzi tangulizi kuhusu tofauti ya dhana ya viegesho na vijalizo kwa mtazamo wa Nadharia ya Eksibaa. Katika Kiswahili viegesho vya kiwango huundwa na aina mbili tu za virai ambavyo ni baadhi ya virai vielezi na virai vihusishi kama ifuatavyo:

**Virai Vihusishi na Viegesho vya Kiwango**
Aina ya kwanza ya viegesho vya kiwango ni baadhi ya virai vihusishi vinavyounda viegesho vya kiwango. Vihusishi ni aina ya maneno ambayo huhusisha neno moja na lingine/kirai kimoja na kingine au hata kishazi na kishazi (Obuchi & Mukhwana, 2015). Vihusishi huungana na nomino kuunda virai vihusishi. Maneno kama *ya, la, cha, pa, mwa, na, wa, vya, za, kwa, katika, -enye, hadi, mpaka, tokea, kuanzia, tangu, bila, kama, kutoka, karibu, hata, angalau* na mengineyo huungana na

nomino kuunda virai vihusishi mbalimbali. Mfano, *Juma anacheza mpira kwa nguvu.*

**Juma anacheza mpira *kwa nguvu***




Katika kielelezo hapo juu, (KN + KT + KH) ni vipashio vinavyounda sentensi (*Juma anacheza mpira kwa nguvu*). Katika mfano huu kiambajengo (*kwa nguvu*) ni kirai kihusishi kinachoundwa na kihusishi (*kwa*) na nomino (*nguvu*).

Virai vihusishi vingi vinavyoundwa na kihusishi (*kwa*) ndiyo vinavyoongoza katika lugha ya Kiswahili kama viegesho vya kiwango. Imebainika pia, kuwa virai vihusishi vinavyoundwa na vihusishi vya –a unganifu (*ya, la, za, wa* na kadhalika) huwa ni vijalizo na siyo viegesho. Vifuatavyo ni virai vihusishi vinavyounda viegesho vya kiwango:

**Jedwali Na. 01: Virai Vihusishi vya Viegesho vya Kiwango**

| | | | |
|---|---|---|---|
| *Kwa wingi* | *Kwa kadiri* | *Kwa kiwango* | *Kwa kina* |
| *Kwa kawaida* | *Kwa kiasi* | *Kwa hali* | *Kwa mara* |
| *kwa idadi* | *Kwa wastani* | *Kwa asilimia* | *Kwa ujumla* |
| *Kwa baadhi* | *Kwa upana* | *Kwa uhakika* | *Kwa utoshelevu* |
| *Kwa ukubwa* | *Kwa uchache* | *Kwa pigo moja* | *Karibu asilimia* |
| *Katika kiwango* | *Kwenye idadi* | *Hata kidogo* | *Kuanzia mwanzo* |
| *Kutoka kwa mmoja wao* | | | |

Chanzo cha Data: Mtafiti (2020)

Katika jedwali la kwanza hapo juu, ni aina ya kwanza ya viegesho vya kiwango vinavyoundwa na virai vihusishi vinavyoundwa na kihusishi pamoja na nomino ya kiwango.

**Jedwali Na. 02: Virai Vihusishi vya Viegesho vya Kiwango**

| | |
|---|---|
| *Kwa utendaji uliotukuka* | *Kwa undani Zaidi* |
| *Kutoka namba ya kwanza* | *Kwa uwezo mkubwa* |
| *Kwa ukweli uliotosheleza* | *Kwa ukali wa ajabu* |
| *Kwenye kundi la kwanza* | *Angalau mara moja* |
| *Kuliko ufaulu wa kwanza* | *Kutoka fungu dogo* |
| *Kuanzia namba ya kwanza* | |


Chanzo cha Data: Mtafiti (2020)

Jedwali la pili ni aina ya pili ya viegesho vya kiwango vinavyoundwa na virai vihusishi vinavyoundwa na kihusishi pamoja na nomino inayopata ukiwango kutoka katika kipashio kinachoijaliza.

**Viegesho vya Kiwango Vinavyoundwa na Virai Vihusishi vyenye Nomino ya Kiwango**

Kama katika maelezo yaliyotangulia kuwa, aina hii ya virai vihusishi vya viegesho vya kiwango ni virai vihusishi vinavyoundwa na kihusishi pamoja na nomino ya kiwango. Tuchunguze mfano ufuatao:


**Kielelezo Na. 06: Mfano wa Kiegesho**
**Kwa nguvu mno, mtoto amesukuma mlango**




Katika kielelezo Na. 06, kiegesho cha kiwango ni kiambajengo KH (*kwa nguvu mno*) kwa kuwa ni kiambajengo kinachoshirikiana tu na kiambajengo cha kati, S′ (*mtoto amesukuma mlango*) kukiongezea taarifa kiambajengo cha juu. Kiegesho cha kiwango (KH) kimeundwa na kihusishi (*kwa*) na kijalizo chake ambacho ni nomino (*nguvu*) ambayo ni nomino ya kiwango, kwa kuwa inataja wazi uzito uliotumika kusukuma mlango.

Mchoroti huo unaweza kufafanuliwa zaidi kwa kutumia kanuni za kisintaksia za ubainishaji wa virai. Hii itasaidia kuweka wazi uhusiano wa hiari na uhusiano wa lazima na hatimaye kubainika wazi kiegesho cha kiwango kama ifuatavyo:

**Kanuni Na. 01: Ubainishaji wa Viegesho**





Katika kanuni hii ya kisintaksia ya kubainisha virai, sentensi (*kwa nguvu mno, mtoto amesukuma mlango*) imeundwa na virai vikuu viwili (KN + KT). Ndani ya kirai kitenzi (KT) ndipo panapopatikana kiegesho ambacho ni kirai kihusishi (KH) ambacho kinashirikiana tu na kirai kitenzi cha kati (T′) kuunda kirai kitenzi kikuu. Kirai kihusishi (KH) kimeundwa na kihusishi (H) na kirai nomino (KN), nomino inayounda kirai nomino hicho ni nomino ya kiwango (nguvu).

**Viegesho vya Kiwango Vinavyoundwa Virai Vihusishi vyenye Nomino yenye Kijalizo cha Kiwango**

Kama maelezo yaliyotangulia awali kuwa, aina nyingine ya viegesho vya kiwango ni virai vihusishi vinavyoundwa na kihusishi pamoja na nomino inayojalizwa na viambajengo vinavyochanuza ukiwango. Tuchunguze mfano ufuatao:

**Kielelezo Na. 07: Mfano wa Kiegesho**


**Mwalimu mkuu amepewa zawadi *kwa utendaji uliotukuka kazini***



Kielelezo hapo juu ni mchoroti unaofafanua kiegesho cha kiwango (*kwa utendaji uliotukuka kazini*). Kiegesho hicho ni kirai kihusishi ambacho ni kirai cha ziada kimuundo kinachoshirikiana na kirai cha kati T′ (*amepewa zawadi*) kuongezea taarifa ya ziada katika kirai cha juu T′ kuunda kirai kikuu (KT). Kiegesho cha kiwango (KH) kimeundwa na kihusishi (*kwa*) pamoja na kijalizo chake ambacho ni kirai nomino (*utendaji uliotukuka kazini*). Kirai nomino hicho kimeundwa na nomino (*utendaji*) pamoja na kijalizo chake ambacho ni sentensi iliyoshushwa hadhi kwa kuwekewa urejeshi (*uliotukuka kazini*). Sentensi hiyo iliyoshushwa hadhi ndiyo yenye kuchanuza ukiwango kwa kutumia kitenzi chake (*tukuka*) kinachorejelea ubora wa kiwango cha juu. Hivyo, nomino (*utendaji*) imeambukizwa ukiwango kutoka katika kijalizo chake na kusababisha kirai nomino chote kuchanuza ukiwango.

Ili kukiweka wazi kiegesho hicho cha kiwango, mchoroti huo unaweza kufafanuliwa zaidi kwa kutumia kanuni za kisintaksia za ubainishaji wa virai, ili kuweka wazi uhusiano wa hiari na uhusiano wa lazima na hatimaye kubainika wazi kiegesho cha kiwango kama ifuatavyo:

**Kanuni Na. 02: Ubainishaji wa Viegesho**




Katika kanuni hii ya kisintaksia ya kubainisha virai, sentensi (Mwalimu mkuu amepewa zawadi *kwa utendaji uliotukuka kazini*) imeundwa na virai vikuu viwili (KN + KT). Ndani ya kirai kitenzi (KT) ndipo panapopatikana kiegesho ambacho ni kirai kihusishi (KH) ambacho kinashirikiana tu na kirai kitenzi cha kati (T′) kuunda kirai kitenzi kikuu. Kirai kihusishi (KH) kimeundwa na kihusishi (H) na kirai nomino (KN). Nomino inayounda kirai nomino hicho ni (*utendaji*) ambayo imejalizwa na sentensi iliyoshushwa hadhi kwa kuwekewa urejeshi (*uliotukuka kazini*) ambayo ndiyo inayosababisha kirai kihusishi chote kiwe na ukiwango.

**Viegesho vya Kiwango vinanvyoundwa na Virai Vielezi**

Aina nyingine ya viegesho vya kiwango ni vile vinavyoundwa na baadhi ya virai vielezi. Vielezi ni aina ya maneno ambayo kwa kawaida hueleza zaidi kuhusu tendo, tukio au hali (Matei, 2008). Kisintaksia, virai vielezi vingi hujitokeza katika mahusiano ya hiari na huwa na kazi ya kutoa taarifa za ziada katika virai au sentensi ambavyo ndivyo huitwa viegesho. Kwa kiwango kikubwa virai vielezi vingi katika Kiswahili ni viegesho, ingawa vipo baadhi ya vielezi vichache sana vinavyojaliza maneno au virai na kuwa vijalizo badala ya viegesho. Katika kuthibitisha maelezo haya, data zifuatazo zinaweza kuthibitisha tofauti ya virai vielezi ambavyo ni viegesho na virai vielezi ambavyo ni vijalizo kama ifuatavyo:


| | |
|---|---|
| a) | Mwalimu anafundisha *mara kwa mara* somo la Kiswahili |
| b) | Mwanafunzi mrefu *sana* anaitwa na mwalimu |

Chanzo cha Data: Mtafiti (2020)

Katika data hapo juu, mfano wa kwanza (a) una kirai kielezi kilichoandikwa kwa hatimlazo (*mara kwa mara*), ambacho kinashirikiana na virai vingine kuunda tungo nzima. Kirai kielezi (*mara kwa mara*) kinaongeza taarifa za ziada tu katika muundo wa tungo hiyo; hivyo, kipo katika mahusiano ya hiari katika muundo huo. Kwa hiyo, kirai kielezi (*mara kwa mara*) katika muundo huo ni kiegesho. Data hiyo inaweza kufafanuliwa zaidi kwa kupitia katika vielelezo vifuatavyo:

**Kielelezo Na. 08: Mfano wa Kiegesho**

**Mwalimu anafundisha *mara kwa mara* somo la Kiswahili**





Katika kielelezo kilichopo juu, kirai kielezi (*mara kwa mara*) ni kiegesho kwa kuwa kipo katika mahusiano ya hiari. Hii ni kwa sababu, kirai kielezi katika mfano huo ni kirai kinachoshirikiana na kirai cha kati T′ (*anafundisha somo la Kiswahili*) kuunda kirai cha juu T′ kwa kuongeza taarifa za ziada katika muundo huo.

Lakini katika mfano wa pili, kirai kielezi kilichoandikwa kwa hatimlazo (*sana*), kinaongeza taarifa za lazima katika kivumishi (*mrefu*) ili kuweza kubainisha


mwanafunzi husika katika muundo wa tungo hiyo. Kwa hiyo, kirai kielezi hicho kipo katika mahusiano ya lazima katika muundo huo. Tufafanue zaidi kwa kutumia kielelezo kifuatacho:

**Kielelezo Na. 09: Mwanafunzi mrefu *sana* anaitwa na mwalimu**




Katika kielelezo hiki, viambajengo vyote vinavyounda sentensi hii vimeainishwa uhusiano wake kati ya kimoja na kingine. Sentensi hii (Mwanafunzi mrefu *sana* anaitwa na mwalimu) imeundwa na virai vikubwa viwili, kirai (KN) na kirai kitenzi (KT). Katika kirai nomino (*mwanafunzi mrefu sana*) ndipo kuna kirai kielezi (*sana*) kinachokusudiwa ambacho kimebebwa katika kirai kivumishi (*mrefu sana*). Katika mchoroti huu, tumechukua tu kirai nomino (KN) ili tufafanue zaidi kijalizo (*sana*).

**Kielelezo na. 10: Mwanafunzi mrefu *sana***



Katika kielelezo Na. 10, kirai kielezi (KE) ni kiambajengo binti kilichozaliwa kutoka katika kiambajengo mama (V′). Hivyo, kinaungana na kutegemeana na kiambajengo dada (V) kuunda kiambajengo mama hicho. Kwa hiyo, (KE + V) ni viambajengo tegemezi vinavyotegemeana katika taarifa ya msingi katika kiambajengo mama hicho. Hivyo, kirai kielezi hicho (*sana*) ni kijalizo cha kivumishi (*mrefu*) na siyo kiegesho.

Imebainika kuwa, virai vielezi vifuatavyo hujitokeza katika miundo mbalimbali kama viegesho vya kiwango:


**Jedwali Na. 03: Virai Vielezi vya Viegesho vya Kiwango**

| | | |
|---|---|---|
| *Mara kwa mara* | *Mara zote* | *Mara moja* |
| *Maradufu* | *Zaidi ya mara moja* | *Zaidi ya idadi ilivyo* |
| *Sanasana* | *Tikatika* | *Fofofo* |
| *Tikitiki* | *Kwanza* | *Mwisho* |
| *Kijumla* | *Kiupekee* | *Kiwastani* |
| *Kiuchache* | *Kiasi cha* | |

Chanzo cha Data: Mtafiti (2020)

Imebainika kuwa virai vielezi vya viegesho vya kiwango vinaweza kuwa virai vielezi vya mara na vijalizo vyake, virai vielezi vya zaidi na vijalizo vyake na baadhi ya virai vielezi vya uradidi. Vingine ni baadhi ya virai vielezi vinavyoundwa na ki- mwanzoni na virai vielezi vya namba. Tuchunguze mfano mmoja kutoka katika virai hivyo kama ifutavyo:

**Kielelezo Na 11: Mtoto anacheza mpira *mara kwa mara***





Katika kielelezo Na. 11, kirai kielezi (*mara kwa mara*) ni kiegesho kwa kuwa kipo katika mahusiano ya hiari. Hii ni kwa sababu kirai kielezi katika mfano huo ni

kirai kinachoshirikiana na kirai cha kati T′ (*anacheza mpira*) kuunda kirai cha juu T′ kwa kukiongezea taarifa za ziada kirai hicho cha juu ili kuunda kirai kikuu (KT).

Ili kukiweka wazi kiegesho hicho cha kiwango, mchoroti huo unaweza kufafanuliwa zaidi kwa kutumia kanuni za kisintaksia za ubainishaji wa virai, ili kuweka wazi uhusiano wa hiari na uhusiano wa lazima na hatimaye kubainika wazi kiegesho cha kiwango, kama ifuatavyo:

**Kanuni Na. 03: Ubainishaji wa Viegesho**




Katika kanuni hii ya kisintaksia ya kubainisha virai, sentensi (Mtoto anacheza mpira *mara kwa mara*) imeundwa na virai vikuu viwili (KN + KT). Ndani ya kirai kitenzi (KT) ndipo panapopatikana kiegesho ambacho ni kirai kielezi (KE) kinachoshirikiana tu na kirai kitenzi cha kati (T′) kuunda kirai kitenzi kikuu. Kirai kielezi (KE) kimeundwa na kielezi (E) na kirai kihusishi (KH).

**Uchambuzi wa Miundo ya Viegesho vya Kiwango**

Nadharia ya Eksibaa kwa kupitia kanuni ya miundo virai, inabainisha miundo ya virai kwa kupambanua neno kuu na vijalizo vyake (XP =X au X + KIJ...). Hii ikiwa na maana kwamba KT inaweza kuundwa na T, au T + KIJ... na kadhalika (Black, 1999). Kwa hiyo, katika taaluma ya sintaksia, tunachunguza namna viambajengo viliundwa kutokana na mpangilio katika sentensi. Kwa kutumia Nadharia ya Eksibaa imebainika kuwa virai vielezi na virai vihusishi vinavyounda viegesho vya kiwango vina miundo tofauti kama inavyooneshwa katika jedwali Na. 04:


**Jedwali Na. 04: Miundo ya Virai Vihusishi Vinavyounda Viegesho vya Kiwango**

| NA | MUUNDO WA KIEGESHO CHA KIWANGO |
|---|---|
| 1 | Muundo wa Kirai Kihusishi chenye Ushikamani wa Kihusishi na Kirai Nomino pekee |
| 2 | Muundo wa Kirai Kihusishi chenye Ushikamani wa Kihusishi, Kirai Nomino na Kirai Kielezi |
| 3 | Muundo wa Kirai Kihusishi chenye Ushikamani wa Kihusishi, Kirai Nomino na Kirai Kivumishi |
| 4 | Muundo wa Kirai Kihusishi chenye Ushikamani wa Kihusishi, Kirai Kivumishi na Kirai Kielezi |
| 5 | Muundo wa Kirai Kihusishi chenye Ushikamani wa Kihusishi, Kirai Nomino na Kirai Kihusishi |
| 6 | Muundo wa Kirai Kihusishi chenye Ushikamani wa Kihusishi, Kirai Nomino na Kishazi Rejeshi |
| 7 | Muundo wa Kirai Kihusishi chenye Ushikamani wa Vihusishi Viwili Pamoja |

Chanzo cha Data: Mtafiti (2020)

Katika data hiyo, tuchukue mfano mmoja tu kwa lengo la kuuchambua na kuufafanua zaidi kwa niaba ya mifano iliyobaki. Muundo wa kirai kihusishi chenye ushikamani wa kihusishi, kirai nomino na kirai kivumishi (KH= H'[ H + KN] N' [N + KV]). Katika muundo huu, kirai kivumishi huwa kinabebwa na kumilikiwa na kirai kihusishi. Tuchunguze Mfano ufuatao katika kielelezo Na 12:


**Kielelezo Na. 12: Wamemiminika uwanjani *kwa idadi kubwa***




Katika kielelezo hapo juu, kiegesho cha kiwango ni kirai kihusishi (*kwa idadi kubwa*) ambacho kipo katika mahusiano ya hiari. Kiegesho hicho cha kiwango ambacho ni kirai kihusishi (*kwa idadi kubwa*) kimeundwa kwa ushikamani wa kihusishi (H), kirai nomino (KN) na kirai kivumishi (KV). Hivyo, kirai kihusishi kinaundwa na kihusishi kinachojalizwa na kirai nomino, pamoja na kirai kivumishi

kinachotoa taarifa za ziada katika muundo huo. Muundo huu unaweza kufafanuliwa zaidi kwa kutumia kielelezo kingine kifuatacho:

**Kielelezo Na. 13: Kwa idadi kubwa**




Katika mchoroti huu, kiegesho cha kiwango kimeundwa na kirai kihusishi (*kwa idadi kubwa*) chenye ushikamani wa kihusishi (*kwa*) kinachojalizwa na kirai nomino (*idadi kubwa*) ambacho nacho kinajalizwa na kirai kivumishi (*kubwa*), yaani (KH= H'[ H + KN] N' [N + KV]).

Kanuni ya kisintaksia ya kubainisha ushikamani wa virai itaweka wazi muundo huu kwa kufafanua viambajengo vinavyounda kiegesho cha kiwango kama ifuatavyo:

**Kanuni Na. 04: Ubainishaji wa Viegesho**

S (KN (N'(N)), KT (T' (T + KN) KH)) — Muundo wa sentensi

KH (H' (H + KN (N' (N + KV)))) — Muundo wa kiegesho cha kiwango

XP (P' (P + XY (Y' (Y + XZ)))) — Kanuni ya muundo wa kiegesho cha kiwango

Kiegesho cha kiwango (*kwa idadi kubwa*) ni kiegesho kimoja chenye viambajengo vitatu ambavyo ni kihusishi (*kwa*), kirai nomino (*idadi kubwa*) na kirai kivumishi (*kubwa*). Hivyo, muundo wa kiegesho cha kiwango (KH) unatokana na ushikamani wa kihusishi (H) na kirai nomino (KN), ambacho kinakumushwa na kirai kivumishi (KE). Miundo mengine ni ya virai vielezi vinavyounda viegesho vya kiwango kama ifuatavyo:


**Jedwali Na. 05: Miundo ya Virai Vielezi Vinavyounda Viegesho vya Kiwango**

| NA | MUUNDO WA KIEGESHO CHA KIWANGO |
|---|---|
| 1 | Muundo wa Kirai Kielezi Pekee |
| 2 | Muundo wa Kirai Kielezi chenye Ushikamani wa Kielezi na Kirai Kihusishi |
| 3 | Muundo wa Kirai Kielezi chenye Ushikamani wa Kielezi na Kirai Kivumishi |
| 4 | Muundo wa Kirai Kielezi chenye Ushikamani wa Kielezi na Sentensi jalizi |
| 5 | Muundo wa Kirai Kielezi chenye Ushikamani wa Kielezi, Kirai Nomino na Kirai Kihusishi |
| 6 | Muundo wa Kirai Kielezi chenye Ushikamani wa Kielezi na Kirai Kielezi |
| 7 | Muundo wa Kirai Kielezi chenye Ushikamani wa Kielezi, Kirai Kivumishi na Kirai Kielezi |

Chanzo cha Data: Mtafiti (2020)

Katika data hiyo, tuchukue mfano mmoja tu kwa lengo la kuuchambua na kuufafanua zaidi kwa niaba ya miundo iliyoorodheshwa katika jedwali. Muundo wa kirai kielezi chenye ushikamani wa kielezi, kirai nomino na kirai kihusishi (KE= (E' [E+ KN] KH). Katika muundo huu, kirai nomino huwa kinabebwa na kumilikiwa na kirai elezi, ilhali kirai kihusishi nacho huwa kinabebwa na kumilikiwa na kirai nomino. Tuchunguze mfano ufuatao:


**Kielelezo Na 14:** ***Mara moja kwa wiki*****, wanafunzi wa kidato cha nne wa shule ya Mpendae huwa wanafanya mtihani wa ndani**




Katika data hii kwenye kielelezo hapo juu, kiegesho cha kiwango ni kirai kielezi (*mara moja kwa wiki*) ambacho kimejitokeza katika mahusiano ya hiari. Hii ni kwa sababu kirai kielezi katika data hii ni kiambajengo kinachoshirikiana na

kiambajengo S′ (*wanafunzi wa kidato cha nne wa Shule ya Mpendae huwa wanafanya mtihani wa ndani*) kuongeza taarifa katika sentensi (S). Hivyo, kiegesho cha kiwango (*mara moja kwa wiki*) ni kirai kielezi ambacho kimeundwa kwa ushikamani wa kielezi kinachojalizwa na kirai nomino pamoja na kirai kihusishi kinachokumusha kirai elezi chote, kama inavyooneshwa katika kielelezo kingine hapa chini.

**Kielelezo Na. 15: Mara moja kwa wiki**




Katika kielelezo Na. 15, kiegesho cha kiwango (*mara moja kwa wiki*) ambacho ni kirai kielezi kimeundwa kwa ushikamani wa kielezi (*mara*) chenye kijalizo ambacho ni kirai nomino (*moja*). Kirai elezi hicho nacho kinakumushwa na kiegesho ambacho ni kirai kihusishi (*kwa wiki*), yaani KE = (E' [E + KN] KH).

Kwa ufupi, kanuni ya kisintaksia ya kubainisha ushikamani wa virai itaweka wazi muundo huu kwa kufafanua viambajengo vinavyounda kiegesho cha kiwango kama ifuatavyo:

**Kanuni Na. 05: Ubainishaji wa Viegesho**

$S\{KE, \{KN, KT\{T'\{T+KN\}\}\}\}$ — Muundo wa sentensi

$KE\{E'\{E+KN\}KH\}$ — Muundo wa kiegesho cha kiwango

$XP\{P'\{P+XY\}XZ\}$ — Kanuni ya muundo wa kiegesho cha kiwango

Kanuni hii ya ushikamani wa virai inabainisha miundo ya virai katika sentensi. Kwa hiyo, kwa mujibu wa kanuni hii, muundo wa kiegesho cha kiwango (KE) unatokana na ushikamani wa kielezi (E) kinachojalizwa na kirai nomino (KN). Kirai kielezi hicho kinapata taarifa za ziada kutoka katika kirai kihusishi (KH) kinachoundwa na kihusishi na kijalizo chake ambacho ni kirai nomino.

**Hitimisho**

Katika makala hii, miundo ya viegesho vya kiwango katika sentensi za Kiswahili imechunguzwa, imebainishwa na kufafanuliwa. Makala imefafanua dhana ya viegesho, tofauti ya viegesho na vijalizo, ujitokezaji wa viegesho katika sentensi pamoja na miundo ya viegesho. Mjadala katika makala hii umebainisha kuwa katika lugha ya Kiswahili, viegesho vya kiwango vina miundo tofauti kutoka katika virai vihusishi na virai vielezi.

Makala haya yameweka wazi miundo kumi na nne (14) ya viegesho vya kiwango inayotokana na ushikamani wa virai vinavyounda viegesho hivyo. Muundo wa kirai kihusishi chenye ushikamani wa kihusishi na kirai nomino, muundo wa kirai kihusishi chenye ushikamani wa kihusishi, kirai nomino na kirai kielezi ni miundo iliyofafanuliwa. Miundo mingine ni muundo wa kirai kihusishi chenye ushikamani wa kihusishi, kirai nomino na kirai kivumishi na muundo wa kirai kihusishi chenye ushikamani wa kihusishi, kirai nomino, kirai kivumishi na kirai kielezi.

Pia, miundo mingine ni muundo wa kirai kihusishi chenye ushikamani wa kihusishi, kirai nomino na kirai kihusishi na muundo wa kirai kihusishi chenye ushikamani wa kihusishi, kirai nomino na kishazi rejeshi imefafanuliwa. Aidha, kuna miundo mingine ya viegesho vya kiwango ambayo ni muundo wa kirai kihusishi chenye ushikamani wa vihusishi viwili pamoja na kijalizo. Pia, kuna miundo ya kirai kielezi pekee, kirai kielezi chenye ushikamani wa kielezi na kirai kivumishi na kirai kielezi chenye ushikamani wa kielezi na kirai kivumishi.

Miundo mingine ni kirai kielezi chenye ushikamani wa kielezi, kirai nomino na kirai kihusishi; pia, kuna muundo wa kirai kielezi chenye ushikamani wa kielezi na kirai kivumishi. Mwisho ni muundo wa kirai kielezi chenye ushikamani wa kielezi na sentensi jalizi na muundo wa kirai kielezi chenye ushikamani wa kielezi, kirai kivumishi na kirai kielezi.

**Marejeleo**

Arts, B. (1977). *English Syntax and Argumentation*. London: Mcmillan Press.

Black, A. C. "*A Step – by – Step Introduction to the Gorvement and Binding Theory of Syntax.*" (http://www.sil.org/Americas/Mexico/ling/E002-Intro GB. Pdf [Februari, 1999]).Imepakuliwa tarehe 24-10-2020

Chomsky, N. (1955). *The Logical Structure of Linguistic Theory*. Ms. Hervard: Hervard University na MIT. (Toleo lililorudiwa na kuchapishwa na Plenum, New York, 1975).

Chomsky, N. (1957). *Syntactic Structures*. Hauge: Mouton Publisher.

Chomsky, N. (1970). "Remarks on Nominalization". Katika Jacobs, R. na Rosenbaum, P. (Wah.) *Readings in English Transformational Grammar*, uk 62-67, Waltham: Ginn Publisher.

Chomsky, N. (1981). *Lectures on Gorverment and Binding*. Dordrecht: Foris.

Chomsky, N. (1982). *Some Concepts and Consequences of the theory of Gorverment and Binding*. Chicago: MIT Press.

Chomsky, N. (1995). *Bare Phrase Structure Gorverment and Binding Theory and the Minamalist Program*. Kimehaririwa na Webelhuth, G. Oxford: Blackwell.

Dembetembe, N.C. (1987). *A Linguistic Study of the Verb in Korekore*. Harare: Heram University.

Dowty, D. (1997). *Adjunct-to-Argurment Reanalysis in Dynamic Theory of Grammar: The Problem of Prepositions*. Makala iliyowasilishwa kwenye kongamano la uchunguzi wa maana la Blaubeuren, Chuo Kikuu cha Tubingen: Tarehe 02 Machi, 1997.

Dowty, D. (2000). "The Dual Analysis of Adjuncts/Complements". Katika *Categorial Grammar's Scientific Contribution*. Juz. 09, uk 20-27. Ohio: State University State.

Enrst, T. (2004). *The Syntax of Adjuncts*. Cambridge: Cambridge University Press.

Freidin, R. (1992). *Foundations of Generative Grammar*. Cambridge: MIT Press.

Haegeman, L. (1991). *Introduction to Gorvement and Binding*. Oxford: Blackwell Publishers.

Haegeman, L. (1994). *Introduction to Gorvement and Binding*. (Toleo la Pili). Oxford: Blackwell Publishers Ltd.

Harries, L. (1969). Adjuncts in Swahili. Katika: *Jarida la Chuo cha Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili*, Juz. 39. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Huddleston, R na Pullum, G.K. (2006). *A student's Introduction to English Grammar* (Toleo la pili). New York: United Kingdom at the University Press.

Matei, A.K. (2008). *Darubini ya Sarufi: Ufafanuzi Kamili wa Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Maw, J. (1969). *Sentences in Swahili, A study of Internal relationships*. London: School of Oriental Studies.

Mgonja, L. E. I. (1985). "Adjunct in Swahili". Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Newmayer, F. J. (1986). *Linguistic Theory in America.* (Toleo la Pili). Orlando: Academic Press.

Obuchi, M. S. na Mukhwana, A. (2015). *Muundo wa Kiswahili, Ngazi na Vipengele*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation Printing Services Ltd.

Radford, A. (1988). *Transformational Grammar*. Cambridge: Cambridge University Press.

Tallerman, M. (2005). "The Celtic Languages". Katika Guglielimo Cinque na Richard S, Kayne. *The Oxford Handbook of Comparative Syntax*, *uk. 839-79*. Oxford: Oxford University Press.

Van Vallin, R. D. (2001). *An Introduction to Syntax*. Cambridge: Cambridge University Press.